OFISI YA RAISI – TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

SHULE YA SEKONDARI MWAMAGIGISI

S.L.P 39, SIMIYU – WILAYA YA BUSEGA

Mawasiliano: +255 784 760 678 / +255 763 816 298

Kumb Na._____ **Tarehe _____/ _____/ _____**

Jina la Mwanafunzi _____

S.L.P _____

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWAMAGIGISI WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021.</u>

1.0 UTANGULIZI

Nina furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **<u>KWANZA</u>** katika shule hii mwaka **<u>2021</u>** Shule ya sekondari Mwamagigisi ipo umbali wa Km 35 Mashariki mwa makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya Busega. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **<u>11/01/2021.</u>** Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **<u>11/01/2020</u>** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **<u>18/01/2021</u>** ndani ya siku saba.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. Sare za Shule

(a) Sare ya shule hii ni suruali **DARK BLUE** mbili (02) zenye mifuko mitatu, marinda mawili kila upande kwenye mifuko ya mbele, upana chini ni Sm 16 kwa wavulana. NB: **suruali isiwe modal** na sketi **DARK BLUE** mbili (02) zenye marinda ya kupangana mfuko mmoja kwa wasichana na ifike kwenye vifundo vya miguu.
Aina ya kitambaa kimeambatanishwa. Viatu vyeusi vyenye Kamba, soksi nyeupe kwa wavulana na wasichana

(b) Rangi ya Hijabu ifanane na sare za shule

(c) Sare za michezo kwa shule ni:-

(i) T –shirt (nyekundu iliyoiva kwa wavulana na wasichana)
(ii) Bukta nyekundu ndefu kwa wavulana na wasichana
(iii) Raba nyeupe kwa wavulana na wasichana
(iv) Soksi nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana (Kwa ajili ya michezo)

2.2. VIFAA VYA TAALUMA

(i) Madaftari ya kutosha, (Yako mwenyewe) Nashauri ununue Counter book 10
(ii) Kalamu za wino (Mweusi au Bluu) za kutosha, Kalamu ya risasi (Pencil) na mfuto
(iii) Bofa (Mathematical Set) na vifaa vyake vyote.
(iv) Dictionary kwa ajili ya muongozo wa kujifunza Kiingereza
(v) 4 – figure mathematical table (01) Ya NECTA.
(vi) Mfuko mzuri wa kutosha (School bag) kubebea vifaa vyako – isiwe mifuko ya karatasi

2.3. RATIBA YA SHULE.

Wanafunzi wote wanatakiwa kufika shuleni kwa siku zote za masomo **saa moja kamili (01:00) asubuhi** na kuondoka **saa tisa kamili (9:00) alasiri.** Katika ratiba ya shule kuna muda wa kusafisha mazingira, michezo, shughuli za elimu ya kujitegemea (EK), muda wa mafunzo rekebishi na mambo mengine yakupasayo kufanya kama mwanafunzi.

Masomo yanayofundishwa ni:-

1. Hisabati (Basic mathematics)
2. Kiswahili
3. Kiingereza (English language)
4. Jiografia (Geography)
5. Uraia (Civics)
6. Kemia (Chemistry)
7. Elimu viumbe (Biology)
8. Fizikia (Physics)
9. Historia (History)
10. Fasihi ya lugha (Literature in English)

Mbali na masomo hayo ya darasani, pia kuna vipindi vya kongamano (Debate), vilabu vya masomo, vilabu vya mahusiano ya kijinsia (FEMA), TAKUKURU na Afya.

NB: Shughuli nyingine zinaweza kufanyika baada ya muda wa vipindi vya masomo.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

A: HESHIMA.

(i) Unatakiwa kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
(ii) Hauruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yako na wanafunzi wengine, kwa walimu wako na kwa watu wengine.
(iii) Unapaswa kuheshimu wafanyakazi wote wa shule kama walezi wako
(iv) Kushirikiana na kusaidiana ni jambo la muhimu kwa kila mwanafunzi
(v) Unatakiwa kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote
(vi) Hauruhusiwi kabisa kufanya mambo yafuatayo: -
  (a) Kuvuta sigara
  (b) Kufuga kucha, ndevu, na kuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi.
  (c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
  (d) Kugombana/Kupigana
(vii) Unatakiwa kuitika mara moja na kukimbilia alipo anayekuita.
(viii) Unatakiwa kuheshimu bendera ya taifa, Picha za viongozi wa serikali, Nembo ya Taifa, Wimbo wa taifa na Fedha za Taifa.
(ix) Unatakiwa kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote utakapokuwa
(x) Unatakiwa kunyoosha mkono juu na kusimama unapouliza na kujibu maswali
(xi) Unatakiwa kukaa kimya unapokuwa darasani. Usitoke bila ya ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko darasani.
(xii) Unapaswa kutunza mazingira ya shule katika hali ya usafi ikiwa ni pamoja na kushiriki kupanda na kuhifadhi miti iliyopandwa
(xiii) Kupatikana na simu ya mkononi

B: MAHUDHURIO

(i) Ni lazima mwanafunzi kuhudhuria shule kwa muda wote wa masomo
(ii) Unatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani nan je ya darasa
(iii) Unatakiwa kuhudhruia na kushiriki kazi zote za mikono.
(iv) Unatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi, usafi, kupandisha bendera ya Taifa, n.k.

C: KUWAHI

(i) Unatakiwa kuzoea na kuthamini muda.
(ii) Unatakiwa kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku.
(iii) Unatakiwa kuwahi unaposikia wito wa dharura.
(iv) Unatakiwa kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa.

D: UVAAJI WA SARE YA SHULE

Kutakuwa na sare inayojulikana kwa wanfunzi na jumuiya nzima. Sare inayokubalika na yenye heshima kitaifa. Sare hiyo itavaliwa wakati wote wa :-

(a) Masomo darasani
(b) Wanafunzi wanapotoka nje ya shule kwa shughuli za shule
(c) Mhadhara wa shule (BARAZA)
(d) Wanafunzi wanapokwenda Hospitalini n.k
(e) Utavaa nguo za michezo na kuzitumia wakati wa michezo tu.
(f) Unatakiwa kuwa na vazi la kazi wakati wote wa kazi za mikono
(g) Huruhusiwi kuvaa kofia, viatu vya ghorofa, na mapambo mengine.
(h) Sare ya shule inatakiwa kuwa safi wakato wote
(i) Unatakiwa kuwa na kitambulisho cha shule unaposafiri nje ya shule au likizo.

E: MIPAKA YA SHULE

(i) Hauruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa maalum
(ii) Hauruhisiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalumu.
    (a) Chumba cha walimu
    (b) Ofisi za shule
    (c) Maabara
    (d) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.
(iii) Hauruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo.
    (a) Vilabu vya pombe
    (b) Majumba ya starehe
    (c) Majumba ya kufikia wageni.

F: MAKOSA MAKUBWA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE MARA MOJA.

1. Wizi wa aina yoyote ile.
2. Kuoa / Kuolewa
3. Matusi kwa kiongozi na watu wanaokuzidi umri na walio chini yako
4. Ulevi wa pombe, bangi na madawa ya kulevya.
5. Uasherati.
6. Magonjwa ya zinaa
7. Ugomvi nje na ndani ya shule
8. Kupata / Kusababisha / Kutoa mimba
9. Kosa la jinai lililothibitishwa na mahakama
10. Kuharibu au kuchana picha za viongozi au Bendera ya Taifa
11. Kukataa adhabu ya viranja au walimu
12. Utoro wa aina yoyote ile
13. Kuwa / Kumiliki simu.

G: MASHARTI MENGINE

Jaza Fomu zifuatazo na kuzikabidhi pindi unapolipoti shuleni.

(a) Fomu ya kupima Afya
(b) Fomu ya kukubali sharia za shule
(c) Histori ya Mwanafunzi

MUHIMU: Ni mategemeo yangu kuwa unaelewa ya kwamba shule ni mahali pa kujifunza. Kama unatambua hivyo ndivyo. Walimu na wanafunzi wenzako ndio nyenzo muhimu kwako kupata mafanikio:

MWL. ALHSELMS D.A MAKOMBIJA

_____

MKUU WA SHULE

OFISI YA RAISI – TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
BUSEGA DISTRICT COUNCIL
SHULE YA SEKONDARI MWAMAGIGISI
HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la Mwanafunzi (Majina Matatu)
   _____
2. Shule ya Msingi aliyosoma _____
3. Tarehe ya kuzaliwa: Siku _____Mwezi _____ Mwaka _____
4. Dini / Dhehebu _____
5. Jina la Baba _____
6. Jina la Mama _____
7. Anuani ya Mzazi/Mlezi _____
8. Jina la Mtaa/Kijiji _____
9. Kazi ya Baba _____
10. Kazi ya Mama _____
11. Mahali anapoishi/ Kata ya _____Kijiji_____
    Mtaa _____Balozi_____
12. Unapanga Kijiji/Mtaa_____
13. Unaishi na Mzazi, weka Vema(√) Ndiyo [ ], Hapana [ ] Jina _____
14. Unaishi na Mlezi weka Vema(√) Ndiyo [ ], Hapana [ ] Jina _____
    Unaishi kwa kupanga, weka Vema(√) Ndiyo [ ], Hapana [ ]
15. Kazi ya mlezi _____
16. Anuani ya Mzazi / Simu ya Mzazi _____
17. Hali nyingine ya familia yako _____

JINA LA DADA/KAKA	UMRI	KAZI AIFANYAYO	MAHALI ANAPOFANYIA KAZI AU KUSOMA SHULE

Nathibitisha kuwa taarifa niliyotoa hapo juu ni sahii tupu.

Jina _____

Sahihi _____ Tarehe: _____

OFISI YA RAISI – TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

BUSEGA DISTRICT COUNCIL

SHULE YA SEKONDARI MWAMAGIGISI

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWAMAGIGISI

ANUANI YAKO

_____

S.L.P _____

_____

Tarehe ____/_____/_____

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI MWAMAGIGISI,

S.L.P 39,

BUSEGA.

1. Mimi _____ (Jina la mwanafunzi) Msichana / Mvulana nakubali kujiunga na kidato cha _____ katika shule ya sekondari Mwamagigisi leo tarehe _____/_____/_____ Nitafika shuleni bila kuchelewa. Nitatii sheria za shule na za nchi hii. Nitaishi maisha mazuri, nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii na juhudi katika masomo, kazi za nje na michezo.

   JINA LANGU _____
   SAHIHI YANGU _____ TAREHE _____/_____/_____

2. Mimi _____ (Jina la mzazi / mlezi) nakubali mtotowangu _____ (Jina la mwanafunzi) ajiunge na kusoma katika shule ya Sekondari Mwamagigisi ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote / Mahitaji yote anayotakiwa kufika nayo shuleni kama ilivyotajwa katika barua ya masharti ya kujiunga na shule hii.

   Nitahakikisha ninafuatilia kwa ukaribu mahudhurio, mwenendo, maendeleo ya mtoto wangu shuleni, na sitasita kumwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii.

   JINA LANGU _____
   SAHIHI YANGU _____ TAREHE _____/_____/_____

OFISI YA RAISI – TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

BUSEGA DISTRICT COUNCIL

MWAMAGIGISI SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 39, BUSEGA

FORM FOR STUDENT MEDICAL EXAMINATION

1. Student's Name: _____
2. Age _____
3. Blood examination hemoglobin _____
4. Any abnormalities noted _____
5. Stool examination _____
6. Urinarisis _____
7. T.B. Test (If negative was immunization given) _____
8. Eyes _____
9. Chest _____
10. Abdomen _____
11. Any chronic complaints not noted above _____
12. Asthma _____
13. Headache _____
14. Inability _____
15. Skin diseases _____
16. Pregnancy (For girls) _____
17. Also anything else that the school health staff should know about _____
    _____
18. Any treatment given or recommended: _____

NOTES: If any of the examinations requested above cannot be carried out is useful if it is noted that they have not been rather than writing NAD down.

In case of bilhazia it is recommended that students attend Bilhazia Clinic before they come to school

Doctor's Name: _____

Title / Position Held

_____

Signature: _____ Date _____/_____/_____

Station _____